

JE, KWA NINI MTOTO WANGU NI MCHOKOZI?

NEWCOMER
PARENT
RESOURCE
SERIES

Kupata tunachokitaka na kuhitaji ni sehemu ya maisha, lakini watoto wadogo mara kwa mara hawawezi au hawajui jinsi ya kusema mahitaji na matamania yao kwa njia tulivu kwa kutumia maneno. Wanapokuwa wakikua, watoto hujifunza kudhibiti hisia zao na kuingiliana na wengine kwa njia nzuri. Hata hivyo, hadi hiyo ifanyike, watoto wadogo wanaweza kuwa wachokozi wanapokuwa wakijaribu kujizungumza.

Watoto wanaweza kugonga, kurusha mateke, kuuma au kukamata kitu. Watoto wachanga (umri wa miaka 1-3) wanaweza kugonga, kurusha mateke, kuuma, kukamata kitu, kupiga kelele, kuvuta nywele, kuchuna, kusukuma au kukonganisha kichwa. Watoto wa chekechea (umri wa miaka 3-6) wanaweza kufanya yoyote kati ya mambo haya na wanaweza pia kurusha ngumi, kutema mate na kupiga kelele. Wanaweza pia kutishia, kudhalimu au kuwashambulia wengine. Watoto ambao walilazimishwa kuhama wanaweza kuwa na uwezekano zaidi wa kuwa wachokozi.

Je, ni kwanini Baadhi ya Watoto Wadogo ni Wachokozi?

Kuna sababu nyingi kwa nini watoto ni wachokozi.

- Watoto wanafikiria kwamba kuwa wachokozi kutawasaidia kupata wanachokitaka au kuhitajika kwa haraka.
- Watoto uhisi wana nguvu wakiwa wachokozi. Wanapenda kuona majibu waliyoyasababisha.
- Wanajifunza kujidhibiti. Hawawezi kusubiri au kuelewa sababu, na hawajui njia nyingine ya kushughulikia hisia zao au kupata wanachokitaka.
- Wana hisia kali kwamba hawawezi kudhibiti au kukuelezea kuhusu (hasira, wasiwasi, hofu).
- Wanahitaji kusikilizwa.
- Wanafanya tabia ile moja ambayo ndugu au dada yao mkubwa alifanya.
- Wakati mwingine watoto wachanga wanapenda ngozi wanayouma na nywele wanayovuta.



Uchokozi katika Watoto Ambao Walilazimishwa Kuhama

Baadhi ya watoto ambao walilazimishwa kuhama huenda walifadhaishwa na waliyoyapitia. Huenda wewe na mtoto wako mmeona udhalimu, uhasama au watu mwapendao wakiumizwa. Huenda ulipitia hali hatari ambazo zimeathiri mtoto wako, hata kama ulifanya uwezavyo kumlinda. Mambo kama haya yanaweza kusababisha:

- kutenda kwa njia ya kiwewe, matukio ya uhasama na wengine au na sesere;
- kupigana ili kuponea (akiamini maisha yake yamo hatarini);
- hofu kubwa ya kuwapoteza wazazi wakiachana, kisha kumgonga mzazi akirejea;
- kumgonga, kumuuma, kumrushia mateke au ngumi mtoa huduma wakati wa kuachana na mzazi wake;
- kuwa tuli (kujifanya "amekufa" hadi mtu awe karibu na kisha kumshambulia);
- kula kupita kiasi, kukusanya vitu, kuwagonga au kuwasukuma wengine ili kupata chakula;
- kujiumiza.

Tembelea cmascanada.ca/cnc/parents kwa maelezo zaidi ya lugha mbalimbali ya wazazi



SUPPORTING CHILD CARE IN THE SETTLEMENT COMMUNITY / SOUTIEN DE LA GARDE DES ENFANTS DANS LA COMMUNAUTÉ DE RÈGLEMENT

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada